# KCPE 2006

# KISWAHILI

## SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

**Muda: Saa 1 dakika 4(**

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswal

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaa namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
9. Kwa kila swali 1–50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochag kuwa ndilo jibu.

    **Mfano:**

    **Katika kijitabu cha maswali:**

    **21.** Kamilisha: Kinda ni kwa ndege. — ni kwa chui
    A. Shibli
    B. Kisui
    C. Kinege
    D. Maige

    Jibu sahihi ni B.

    **Katika karatasi ya majibu:**

    **1** (A) (B) (C) (D) **11** (A) (B) (C) (D) **21** (A) ▬ (C) (D) **31** (A) (B) (C) (D) **41** (A) (B) (C) (D)

    Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **21**, kisanduku chenye herufi B ndicho kilichocho kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

Maswali 1 mpaka 15.

**Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Kandamiza hakujua thamani __1__ watoto __2__ siku moja __3__ na ulimwengu. Alizoea kuwatumikisha watoto wadogo kwa __4__ kuwaajiri watu wazima asije akajiumiza kwa kuwalipa mishahara mikubwa. Siku moja mwanawe mmoja ambaye __5__ kuyamudu masomo aliamua kuondoka nyumbani bila kuaga. Kandamiza alipogundua kuwa mwanawe __6__ mjini alihuzunika mno. Moyoni Kandamiza alijua kuwa mtoto huyo __7__ jinsi yeye alivyowafanya watoto wa wengine.

**1.** A. wa B. la C. za D. ya

**2.** A. sasa B. hadi C. tangu D. lau

**3.** A. alipofunzwa B. alikofunzwa C. aliofunzwa D. aliyefunzwa

**4.** A. kuchelewa B. kupenda C. kuchelea D. kupendelea

**5.** A. hawezi B. hakuweza C. hataweza D. hajaweza

**6.** A. ametoroka B. ametoroshwa C. ametorokea D. ametorosha

**7.** A. angetesa B. angemtesa C. angewatesa D. angeteswa

Taifa lolote __8__ wananchi wenye afya. Magonjwa __9__ nchi hasara __10__ __11__ pia huwa mzigo mzito kwa mtu binafsi. __12__ ya magonjwa hutokana na __13__ usafi. __14__ huweza kuzuiwa iwapo wananchi wataitikia wito wa kunadhifisha makazi __15__ .

**8.** A. huhitaji B. hahitaji C. yahitaji D. lihitaji

**9.** A. hailetei B. haileti C. hayaileti D. hayailetei

**10.** A. ajabu B. kamwe C. tu D. naam

**11.** A. bali B. mbali C. na D. ijapokuwa

**12.** A. Baina B. Baadhi C. Kati D. Zaidi

**13.** A. kutodumisha B. kutodumu C. kudumisha D. kudumu

**14.** A. Hii B. Hizi C. Hiyo D. Haya

**15.** A. lao B. yao C. zao D. wao

*Kutoka swali la* **16** *mpaka* **30**, *chagua jibu lililo sahihi.*

**16.** "Ki" imetumiwaje katika sentensi: Mweni alipokuja alinipata nikifyeka.
A. Kuonyesha hali ya masharti
B. Kuonyesha hali ya kukanusha
C. Kuonyesha hali ya kuendelea
D. Kuonyesha hali ya udogo

**17.** Ni sentensi ipi sahihi?
A. Ndizi lililoletwa ni langu
B. Miti zilizopandwa zimeota
C. Zulia iliyonunuliwa ni zuri
D. Wema unaozungumziwa ni huu

**18.** Miongoni mwa sehemu hizi za mwili, ni sehemu ipi iliyo tofauti na zingine?
A. Paja
B. Kiganja
C. Pafu
D. Goti

**19.** Polepole, Vibaya, Alasiri, Njiani, ni
A. Vielezi
B. Vivumishi
C. Nomino
D. Viwakilishi

**20.** Methali inayotoa funzo kuwa: Jambo linaloonekana zito kwa mwingine laweza kuwa rahisi kwako, ni:
A. Bahati ya mwenzio usiilalie mlango wazi
B. Mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi
C. Kila mwamba ngoma ngozi huvutia kwake
D. Ganda la muwa la jana chungu kaona kivuno.

**21.** Sentensi "Asingalikwenda kwake asubuhi asingalimkuta" ina maana kuwa:
A. Hakuenda kwake asubuhi lakini alimkuta
B. Alienda kwake asubuhi lakini hakumkuta
C. Alienda kwake asubuhi na akamkuta
D. Hakuenda kwake asubuhi wala hakumkuta

**22.** Ni maneno yapi ambayo yote ni viunganishi?
A. ila, ingawa, lakini, maadamu
B. huyu, hao, ovyo, na
C. ila; lakini, vizuri, wima
D. ingawa, isipokuwa, zuri, safi

**23.** Kivumishi cha sifa kutokana na kitenzi <u>angaa</u> ni:
A. Angaze
B. Angazi


**24.** $\frac{7}{8}$ kwa maneno ni:
A. Subui nane
B. Thumuni saba
C. Subui
D. Thumuni

**25.** Kisawe cha neno <u>barobaro</u> ni
A. Banati
B. Kijana
C. Mvulana
D. Shaibu

**26.** Nomino <u>habari</u> iko katika ngeli ya:
A. U – Zi
B. I – I
C. U– I
D. I – Zi

**27.** **Tano** ni kwa **Chokaa**. **Kitita** ni kwa
A. Pesa
B. Funguo
C. Ndizi
D. Ngozi

**28.** Haya ni maumbo gani?



A. Pembe tatu, Mche, Duara
B. Pia, Mcheduara, Nusuduara
C. Pia, Mchemraba, Mcheduara
D. Pembe tatu, Pia, Nusuduara

**29.** Chagua usemi halisi ufaao wa:
Bahati alisema kuwa angeenda nyumbani kupumzika
A. "Nimeenda nyumbani kupumzika", Bahati alisema
B. "Niende nyumbani kupumzika", Bahati alisema
C. "Nitaenda nyumbani kupumzika", Bahati alisema
D. "Nilienda nyumbani kupumzika", Bahati alisema

**30.** Yapange maneno yafuatayo kulingana na jinsi yanavyotokea katika kamusi:
(i) *Bandika* (ii) *Beua*
(iii) *Birika* (iv) *Bendika*
A. (i) (iv) (ii) (iii)
B. (iv) (ii) (iii) (i)
C. (ii) (i) (iii) (iv)
D. (iv) (i) (ii) (iii)

*Soma taarifa hii kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.*

Huko Tujueni aliishi mtu kwa jina Mkazeni. Mkazeni alikuwa maarufu katika kutabiri ndoto. Alijulikana pia kwa kuyadadisi mambo yaliyozuka humo kijijini mwao. Kwake kulifurika watu ambao aliwahudumia bila malipo.

Wakati fulani Mkazeni alioteshwa kuwa kulikuwa na magari na matrela ambayo yalikuwa yakisimamishwa humo kijijini. Madereva wake walikuwa watu waliojaa wadudu tele mwilini. Madereva hao walikuwa wakiwalaghai vijana kijijini huku wakiwaachia "zawadi" zilizoleta "vilio". Alipowaeleza wanakijiji wakamcheka na kumwambia, "Sasa nguvu zako za utabiri zinapotea. Utawezaje kufikiria kuwa magari hayo yataleta balaa? Magari hubeba mali!"

Ingawa maneno hayo yalisemwa kiutaniutani, yalimchoma maini, akaamua kufyata ulimi na kukaza nia yake. Alijitahidi kuihimiza aila yake kuhusu umuhimu wa tabia njema.

Siku nyingine tena akaota ndoto kuwa huko Tujueni kumeingia joka kubwa lililowameza vijana wengi. Ingawa wanakijiji walikuwa wamempuuza hapo awali, aliwafafanulia ndoto hiyo nao wakazidi kumcheka. "Sasa tena utabiri umeleta mambo ya nyoka? Tangu uzaliwe umewahi kumwona nyoka kama huyo?" Hapo Mkazeni akaona amedharauliwa kupita kiasi, akaamua "kujimezea" utabiri wake mwenyewe, lake liwe jicho tu. Watu ambao waliamua kutojihadhari kabla ya hatari, angewafanya nini? Kidole kimoja kingevunjaje chawa?

Miaka michache ikapita, nayo magari na matrela ya kikweli yakafika pale na kupafanya kituo cha mapumziko. Madereva wakaiona sehemu hiyo ikiwa na starehe nyingi. Tujueni ikajulikana. Biashara madukani na kwenye masoko zikaongezeka.

Baadhi ya watu waliokuwa wamempuuza Mkazeni wakasema, "Oneni mtabiri yule na ndoto zake. Maafa aliyoyatabiri ni hizi pesa tunazozipata? Alitaka tufe maskini? Muone sasa, amenyamaza jii kama maji ya mtungi. Anasema anaihubiria familia yake isijihusishe na biashara haramu. Biashara gani haramu hapa? Cha kupata si cha kuiba."

Baada ya muda, familia nyingi zikaanza kulia. Utabiri ukaja kutokea kweli. Wadudu walikuwa ni UKIMWI na joka likawa maangamizi yaliyoletwa na madhara ya UKIMWI. Wanakijiji waliathirika na kujuta. Kituo hicho cha biashara kikawa na sifa mbaya. Watu wengi wakafa na biashara ikazidi kufifia.

Mkazeni akawa anasikitishwa na matokeo ya mapuuza na tamaa za wanadamu. Kwake yeye na familia yake waliendelea kuishi vyema kinidhamu.

**31.** Mkazeni alikuwa karimu kwa sababu
- A. alitabiri mambo mengi bila chuki
- B. aliwatabiria watu mambo bila kuwalipisha
- C. watu wengi walimwendea kwa utabiri
- D. watu wengi walimdharau lakini hakulipiza

**32.** UKIMWI ndotoni unaweza kulinganishwa na:
- A. wadudu na joka kubwa
- B. matrela na madereva
- C. madereva wenye wadudu
- D. vijana wenye wadudu

**33.** Wanakijiji wanaposema, "Sasa nguvu zako za utabiri zinapotea" wanamaanisha:
- A. Mkazeni si mtabiri tena
- B. wanaushuku utabiri wa Mkazeni
- C. hawautaki utabiri wa Mkazeni
- D. Mkazeni hutabiri yasiyo ya kweli

**34.** Biashara madukani ziliongezeka kwa sababu
- A. watu wengi walikuja kutafuta utabiri wa Mkazeni
- B. kulikuwa na starehe nyingi katika masoko
- C. Tujueni ilikuwa kituo cha mapumziko cha madereva wa matrela
- D. Tujueni ilijulikana na madereva wa matrela makubwa

**35.** Watu wengi wa Tujueni walikuwa ni:
- A. wenye tamaa na watabiri
- B. wapuuzaji na watabiri
- C. wenye tamaa na malezi bora
- D. wapuuzaji na wenye tamaa

**36.** Kulingana na taarifa hii, UKIMWI uliendelezwa sana na:
- A. madereva wa magari na matrela
- B. wafanyibiashara wenye matrela na magari
- C. madereva wapitiao katika vituo vya biashara
- D. wazazi wenye tamaa ya kupata mali

**37.** Baada ya Mkazeni kupuuzwa **tena** alichukua hatua zipi?
- A. Alitabiri mara ya pili na kungojea matokeo
- B. Alibishana na wapuuzaji na kuwapa matokeo
- C. Aliwaangalia tu waliompuuza na kuendelea kutabiri
- D. Alinyamaza, akaongoza familia na kungoja matokeo.

**38.** <u>Kutojihadhari kabla ya hatari</u> ni sawa na:
- A. kutojitayarisha kukabiliana na tatizo
- B. kutoshughulika na hatari
- C. kutoshughulikia matatizo yajapo
- D. kutoogopa madhara ya tatizo.

**39.** Familia ya Mkazeni ilinusurika kwa kuwa:
- A. ilikuwa ikifundishwa kuhusu utabiri
- B. haikufanya biashara na madereva
- C. ilizingatia maadili na mashauri
- D. Mkazeni alikuwa mtabiri

**40.** Kichwa kifaacho **zaidi** kuelezea kifungu hiki ni:
- A. Mkazeni wa Tujueni na utabiri wake
- B. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu
- C. UKIMWI utaangamiza watu wengi
- D. Mchelea mwana kulia hulia mwenyewe

*Soma taarifa hii kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.*

Maendeleo ya nchi hutegemea mchango na juhudi za kila mwananchi. Hata hivyo ni jambo la kusikitisha kuona kuwa baadhi yetu tuna fikira zisizo za kizalendo kuwa wengine ndio wanaopasa kuiendeleza nchi. Watu wa aina hii hutarajia serikali kuwafanyia hili na lile. Hawathubutu kujiuliza, je, mimi nimeifanyia nini nchi yangu?

Inafaa tukumbuke kwamba nchi ni kama chombo cha usafiri na kila mtu ana wajibu wa kuhakikisha kwamba chombo hicho kimekwenda ipasavyo. Tunahitaji kuwa na bidii za mchwa za kujenga kichuguu. Tuwe na umoja wa nyuki ambao, japo ni viumbe wadogo hudiriki kutengeneza asali ambayo huwafaa wao na kuwalisha binadamu. Ikiwa vidudu hivi vinaweza kuilisha jumuiya, sembuse sisi?

Mungu amemtunukia kila mmoja wetu vipawa anuwai. Ni juu yetu kuvitumia vipawa hivi kuinua uchumi wa nchi. Tukijitahidi pamoja tutaweza kutatua matatizo mengi yanayoikumba nchi. Tukumbuke kwamba kinga na kinga ndipo moto uwakapo. Wananchi katika nyanja mbalimbali hawana budi kuziimarisha nyanja hizi ili kuinua hali zao za maisha. Mathalani, wakulima watumie njia za kisasa za ukulima ili kuzalisha mazao mengi. Wakifanya hivyo, tutaweza kukabiliana na baa la njaa ambalo linawadhuru wananchi wengi.

Vijana nao wana jukumu lao kwa taifa. Wewe kama mwanafunzi, unaweza kuchangia maendelo ya nchi hii kwa kushiriki kikamilifu katika shughuli zote za shule. Ujibidiishe vilivyo, si katika masomo pekee, lakini pia katika michezo. Kwa kuiendeleza michezo ya riadha na hata ya kuigiza, utakuwa umeiendeleza nchi kwa kuukuza utamaduni wako. Isitoshe, unaweza kushiriki katika shughuli za kuzoa taka katika mtaa ulio karibu na shule yako. Ukifanya hivyo utakuwa umeitikia wito wa serikali wa kuhifadhi mazingira.

Sehemu za mashambani zinahitaji kushughulikiwa kimaendeleo. Licha ya kuwa sehemu nyingi zina rutuba, vijana wengi baada ya kupata masomo huhiari kuhamia mijini kutafuta kazi zenye hadhi. Mashamba yameachiwa wazee na bila shaka mazao yamekuwa haba. Hebu tujiulize, je, ikiwa sisi vijana tutaziacha sehemu zetu na kuhamia kwingine, nani atakayeziauni? Je, hatujui kuwa chetu ni chetu na nguo ya kuazima haifai chochote? Ni vyema tukumbuke kuwa ikiwa tunataka kusaidiwa kuendeleza sehemu zetu, ni lazima sisi wenyewe tuwe tayari kuzitumikia kwani abebwaye hujikaza. Mapenzi kwa nchi ni muhimu mno. Shime tuungane kuijenga nchi yetu.

**41.** Maendeleo ya nchi yanahitaji
A. kushughulika kila mara katika kilimo
B. ushirikiano wa kila mwananchi
C. kutotarajia serikali kufanya lolote
D. watu wengine kuendeleza nchi

**42.** Watu walio na fikira za kizalendo ni wale:
A. wanaotarajia kusaidiwa kila mara
B. wanaowataka wengine kushughulikia miradi ya maendeleo
C. wasiojua wameifanyia nini nchi
D. wasiopuuza wajibu wao katika kuendeleza nchi

**43.** Nchi ni kama chombo cha usafiri kwa sababu:
A. wananchi wasipoiendeleza nchi itazorota
B. bila chombo usafiri haufanikiwi
C. wananchi wasiporudi mashambani nchi itazorota
D. bila wasafiri nchi haifanikiwi

**44.** Binadamu wanalinganishwa na nyuki kwani
A. wakiwa na bidii nyingi wanaweza kujifaidi wao na wengine
B. nyuki wana umoja japo ni viumbe wadogo
C. wakiwa na umoja na bidii wanaweza kujifaidi wao na wengine
D. nyuki na mchwa wana bidii za kujenga.

**45.** Katika kifungu, matendo yanayoonyesha ukweli wa methali, "Kinga na kinga ndipo moto uwakapo" ni:
A. vijana kuzoa taka na sote kushiriki katika michezo
B. wote kurudi mashambani na kulima kwa bidii
C. vijana kudumisha utamaduni na kuimarisha elimu
D. ushirikiano wa nyuki na wananchi kujitahidi pamoja

**46.** Kulingana na kifungu, matatizo mengi yatatatuliwa iwapo
A. tutafanya kazi kwa pamoja bila kuzingatia tofauti zetu
B. sote tutakuwa na vipawa tofauti tofauti
C. sote tutajibidiisha katika masomo yetu
D. tutatarajia misaada kuinua hali za maisha yetu.

**47.** Vijana
A. wanapaswa tu kushughulikia masomo
B. wanapaswa kusoma ili kukuza utamaduni
C. wanapaswa kushiriki kuimarisha nchi katika nyanja mbalimbali
D. wanapaswa kushirikiana wao kwa wao kujiinua na kuimarisha kilimo

**48.** Kulingana na kifungu maana ya <u>kazi zenye hadhi</u> ni:
A. kazi zinazolipa mishahara mikubwa
B. kazi zinazofikiriwa kuwa bora kuliko za shambani
C. kazi zenye marupurupu mengi kuliko za shambani
D. kazi za walio na elimu ya juu

**49.** Kulingana na kifungu hiki, <u>abebwaye hujikaza</u> ina maana:
A. unaposaidiwa lazima nawe pia ujitahidi
B. ukibebwa mgongoni usilegee kamwe
C. tusitarajie kusaidiwa bila kusaidia
D. tukiwasaidia wengine lazima tujitahidi

**50.** <u>Ikiwa vidudu hivi vinaweza kulisha jumuiya, sembuse sisi?</u> maana yake ni
A. nyuki wanaweza kulisha watu wengi
B. binadamu ana uwezo wa kushirikiana
C. nyuki wana ushirikiano kuliko binadamu
D. binadamu wana nguvu za kuzalisha kuliko nyuki